



**JARAMOGI OGINGA ODINGA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY**  
**SCHOOL OF EDUCATION, HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**  
**DEPARTMENT OF LANGUAGES, LITERARY AND COMMUNICATION STUDIES**  
**UNIVERSITY EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION**  
**(ARTS) WITH IT**  
**3<sup>RD</sup> YEAR 2<sup>ND</sup> SEMESTER 2023/2024 ACADEMIC YEAR**  
**MAIN CAMPUS**

---

**COURSE CODE: ZLB 9306**

**COURSE TITLE: KISWAHILI PHONOLOGY**

**EXAM VENUE:**

**STREAM: BED-ARTS (REGULAR)**

**DATE:**

**EXAM SESSION: APRIL 2024**

**TIME: 2 HOURS**

---

**Instructions:**

- 1. Answer Question ONE (COMPULSORY) and ANY other 2 questions**
- 2. Candidates are advised not to write on the question paper.**
- 3. Candidates must hand in their answer booklets to the invigilator while in the examination room.**

### **SWALI LA KWANZA (LAZIMA)**

- a) Kwa kurejelea masuala yanayoshughulikiwa, onyesha tofauti kuu kati ya matawi **MAWILI** ya taaluma ya fonolojia. (Alama 8)
- b) Eleza aina kuu **TATU** za sifa majumui za lugha katika taaluma ya fonolojia. Thibitisha majibu yako kwa mifano mwafaka. (Alama 6)
- c) Jadili dhima zozote **TANO** za taaluma ya Fonolojia katika uchambuzi na uchanganuzi wa kiisimu. (Alama 10)
- d) Eleza kikamilifu dhana zifuatazo:
  - i) Kidatu (Alama 2)
  - ii) Silabi (Alama 2)
  - iii) Kiimbo (Alama 2)

### **SWALI LA PILI**

Kwa kutumia mifano kutoka kwa mfumo wa lugha ya Kiswahili, jadili mifanyiko ya kifonolojia ifuatayo:

- a) Kudhoofika kwa konsonanti (Alama 5)
- b) Uchopekaji wa konsonanti (Alama 5)
- c) Mvutano wa irabu (Alama 5)
- d) Uyeyushaji (Alama 5)

### **SWALI LA TATU**

Kwa mifano mwafaka kutoka kwa mfumo wa lugha ya Kiswahili, eleza vigezo **VINNE** vinavyoweza kutumiwa kutambua na kuthibitisha fonimu zake. (Alama 20)

### **SWALI LA NNE**

Fafanua hoja muhimu zinazohusu Nadharia ya Fonolojia Asilia kama inavyotumika katika uchunguzi na uchanganuzi wa lugha. (Alama 20)

### **SWALI LA TANO**

Katika kuifasili dhana ya ‘fonimu’ mitazamo mikuu MITATU imejitokeza. Kwa kuangazia waasisi na hoja kuu zinazojengwa, ijadili mitazamo hiyo. (Alama 20).